# WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI



JARIDA MAALUM

# ZIARA YA MAWAZIRI 8 WA KISEKTA

## YALIYOMO


**01** Mawaziri 8 kutatua migoroto

**02** Mapori yafutwa

**03** Waliopunjwa fidia

**04** Tathmini mpya Mkungunero

**01** Watendaji timizeni wajibu

**02** Hatusajili vijiji

**03** Tabora wanufaika

**04** Sitakuwa kikwazo

**04** Migogoro ni janga kubwa



BODI YA UHARIRI

**MARY MAKONDO**
Mwenyekiti

**LUSAJO MWAKABUKU**
Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini

**WAANDISHI**
Munir Shemweta
Magreth Lyimo
Happiness Shayo



Mji wa Serikali Mtumba, S. L. P. 2908 | 40477- DODOMA | Simu: +255 262 963309/13/14 | Nukushi: +255 262 963316
Barua pepe: ps@lands.go.tz | Tovuti: www.lands.go.tz



Timu ya Mawaziri 8 wa kisekta wakiongozwa na Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi iliyoundwa kushughulikia migogoro ya matumizi ya ardhi ikiwa katika picha ya pamoja na viongozi wa mkoa Tabora

# MAWAZIRI 8 KUTATUA MIGOGORO YA MATUMIZI YA ARDHI VIJIJINI

**NA. LUSAJO MWAKABUKU**
DODOMA WANMM

MAWAZIRI wanane wa kisekta wakioongozwa na Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi wanafanya ziara ya mikoa 10 kutoa matokeo ya utatuzi wa migogoro ya matumizi ya ardhi katika vijiji 975.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dodoma kabla ya kuanza kwa Ziara hiyo, Lukuvi alisema ziara hiyo ni utekelezaji wa maagizo ya Rais Samia Suluhu Hassan kuhusu migogoro ya matumizi ya ardhi kwa vile vijiji ambavyo wananchi wake walivamia maeneo ya hifadhi za misitu, mashamba na mifugo.

Kwa mujibu wa Lukuvi, timu hiyo ya mawaziri wanane itakayoambatana na makatibu wakuu wa wizara za kisekta na wataalamu wa wizara hizo, itaanza kutembelea mikoa 10 kwa awamu ya kwanza na baadaye mengine 16 iliyosalia.

"Kuna baadhi ya hifadhi zimekosa sifa na serikali imeamua wananchi wabaki katika maeneo hayo kwa ajili ya kuendesha shughuli zao na halmashauri kwa kushirikiana na wataalamu zitakuja na zoezi la kupima na kuweka mpango wa matumizi bora ya ardhi ili waishi kwa amani," alisema Lukuvi.

Aliitaja mikoa ambayo mawaziri hao watakwenda kuwa Dodoma watakayoanza katika Wilaya ya Chemba, Singida, Manyara, Tabora, Mbeya, Morogoro, Geita, Mara, Dar es Salaam na Pwani.

Mawaziri watakaokuwa katika ziara hiyo ni kutoka Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Ofisi ya Rais Tamisemi, Kilimo, Mifugo na Uvuvi, Mazingira, Maliasili na Utalii, Ulinzi na Maji.



Timu ya wataalamu kutoka katika wizara zinazoshirikiana katika utatuzi wa hii migogogoro ya matumizi ya ardhi ikitambulishwa kwa wananchi na mwenyekiti wa kamati ya mawaziri ya kisekta Mhe. Lukuvi

"Katika ziara hii, timu yetu ya mawaziri itakutana na viongozi wa mikoa husika ili kupata taarifa mpya kuhusiana na matumizi ya ardhi kwenye vijiji pamoja na kuwatangazia huruma ya Rais ya kuwataka waliovamia maeneo ya hifadhi kubaki kuendesha shughuli zao bila bughudha," alifafanua Lukuvi.

Hata hivyo, Lukuvi alisema kuna baadhi ya maeneo kwenye vijiji hivyo itafanyika tathmini kwa lengo la kuanisha maeneo hatarishi na kusisitiza kuwa maeneo hatarishi wananchi hawatatakiwa kubaki.

Kwa muda mrefu kumekuwa na migogoro ya matumizi ya ardhi kwenye vijiji vilivyokuwa maeneo ya hifadhi ambapo serikali iliombwa kuachia sehemu ya maeneo yaliyovamiwa ili wananchi wake kuendelea na shughuli zao, jambo lililosababisha kuundwa kwa timu maalumu ya mawaziri wa kisekta kwa lengo la kutafuta suluhu ya mgogoro huo.



Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mhe. William Lukuvi akiitambulisha kamati ya Mawaziri 8 wa kisekta kwa wanakijiji wa Kisondoko, Kondoa.

# SERIKALI YAFUTA MAPORI 12 KUWAPATIA WANANCHI




*Waziri wa Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi William Lukuvi akishuka katika helkopta wakati yeye na timu yake ya Mawaziri wa Kisekta walipowasili katika kijiji cha Mwombose wilayani Chemba kuzungumza na wananchi kuhusiana na utatuzi wa migogoro ya ardhi katika maeneo ya hifadhi tarehe 5 Oktoba 2021.*

**Na Munir Shemweta, WANMM DODOMA**

Serikali imefuta mapori 12 yenye ukubwa wa ekari 707, 659 na misitu 12 ya ukubwa wa ekari 46,755 kwa ajili ya kuwapatia wananchi kuendesha shughuli za uzalishaji mali ikiwemo kilimo na ufugaji.

Hayo yamebainishwa leo tarehe 5 Oktoba 2021 jijini Dodoma na Waziri wa Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi William Lukuvi wakati wa mwanzo ziara ya mawaziri nane wa kisekta kutoa mrejesho wa utatuzi wa migogoro ya matumizi ya ardhi katika vijiji 920.

Waziri Lukuvi alisema, tayari GN za Misitu na Mapori hayo zimefutwa katika maeneo husika na sasa taasisi zenye dhamana na maeneo ya hifadhi zinatakiwa kulinda na kuweka alama za mipaka kwenye maeneo yake yaliyobaki kwa lengo la kuepusha kuvamiwa na wananchi.

Kwa mujibu wa Lukuvi, katika vijiji 920 ambavyo timu ya Mawaziri nane itapeleka mrejesho kuhusiana na utatuzi wa migogoro ya matumizi ya ardhi, kwa mkoa wa Dodoma pekee vijiji vyake 40 kati ya 42 vilivyoingia maeneo ya hifadhi havitaondolewa na wananchi wake wataendelea na shughuli zao za kilimo na ufugaji.

Akiwa na timu ya Mawaziri katika kijiji cha Mwombotole Lukuvi alisema, vijiji viwili kati ya 42 katika mkoa huo wa Dodoma itabidi viondolewe kupisha ujenzi wa bwawa la maji la Farkwa na vijiji hivyo ni Bubutole na Mwombose vilivyopo katika wilaya ya Chemba.

Mawaziri nane kutoka wizara za kisekta wameanza ziara katika katika vitongoji vilivyopo vijiji vya Handa na kuzungumza na wananchi wa kitongoji cha Mbugani katika hifadhi ya pori la Swagaswaga na kuendelea na vijiji vya Bubutole na Mwombose kutoa mrejesho ikiwa ni utekelezaji agizo la Rais Samia Suluhu Hassan alilolitoa 7 Agosti 2021 kutaka kutekelezwa kwa ufumbuzi wa migogoro ya matumizi ya ardhi katika vijiji 975 bila kuleta taharuki kwa kuzingatia maslahi mapana ya taifa ambapo mrejesho huo umeanza katika vijiji 920.



*Waziri wa Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi William Lukuvi akizungumza na wananchi wa vijiji vya Bubutole na Mwombose wilayani Chemba mkoani Dodoma wakati wa ziara ya mawaziri wa kisekta kutafuta ufumbuzi wa migogoro ya ardhi katika maeneo ya hifadhi tarehe 5 Oktoba 2021.*



*Sehemu ya wananchi wa vijiji vya wa vijiji vya Bubutole na Mwombose wilayani Chemba mkoani Dodoma wakifuatia maelezo yaliyokuwa yakitolewa na Mawaziri wa kisekta wakati wa ziara ya kutafuta ufumbuzi wa migogoro ya ardhi katika maeneo ya hifadhi tarehe 5 Oktoba 2021.*



*Naibu Waziri wa Malisili na Utalii Mery Masanja akizungumza na wananchi wa vijiji vya Bubutole na Mwombose wilayani Chemba mkoani Dodoma wakati wa ziara ya mawaziri wa kisekta kutafuta ufumbuzi wa migogoro ya ardhi katika maeneo ya hifadhi tarehe 5 Oktoba 2021.*



*Waziri wa Maji Jumaa Awesu akizungumza na wananchi wa vijiji vya Bubutole na Mwombose wilayani Chemba mkoani Dodoma wakati wa ziara ya mawaziri wa kisekta kutafuta ufumbuzi wa migogoro ya ardhi katika maeneo ya hifadhi tarehe 5 Oktoba 2021.*

# WALIOPUNJWA FIDIA KURUDIWA UTHAMINI



Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na mwenyekiti wa kamati ya mawaziri 8 ya kisekta Mhe. William Lukuvi akitoa maelekezo ya namna zoezi la uthamini litakavyorudiwa katika kijiji cha Mombose

**Na. Lusajo Mwakabuku WANMM, Dodoma**

Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na mwenyekiti wa kamati ya mawaziri 8 ya kisekta Mhe. William Lukuvi ameelekeza wakazi wa Kijiji cha Mombose Wilayani Chemba , Dodoma wenye malalamiko ambao walikwisha fanyiwa tahmini na wakalipwa ila hawajaridhika na malipo yao waende kwa mkuu wa wilaya hiyo na vielelezo vyote muhimu kwa ajili ya kuandaliwa mpango wa kufanyika kwa uthamini mpya.

Lukuvi alitoa maelekezo hayo baada ya kupokea malalamiko kutoka kwa baadhi ya wananchi ambao maeneo yao yametwaliwa na serikali katika kijiji hicho lakini malipo waliyolipwa hayaendani na thamani halisi ya maeneo yao.

Wananchi hao walidai kuwa uthamini wa fidia kwa wananchi wa eneo hilo halikufanyika kwa uwazi kwa kuwa, kumekuwa na ulipwaji uliotofautiana viwango kwa maeneo yanayolingana.

Mmoja wa wananchi wa kitongoji hicho ambaye eneo lake limetwaliwa, Bibi Jeniffer Emanuel, aliwasilisha malalamiko yake kuwa alilipwa fidia ya sehemu tu ya eneo lake na kumwomba Waziri Lukuvi kusaidia ili aweze kupata haki.

Bi Jeniffer anadai kuwa yeye alijenga nyumba ya matofali ya kuchoma yenye vyumba vitatu aliyoezeka kwa bati lakini amelipwa fidia ya shilingi Milioni Nne na laki Nane ambayo haiendani na thamani halisi ya nyumba yake

''Kwa mfano huyu mama ni wazi kuwa kazi hapa haijafanyika vizuri kwani kwa jinsi alivyoeleza hiyo nyumba haiendani na kiwango alicholipwa. Hivyo naagiza Mthamini Mkuu wa Serikali aje hapa afanye kazi hiyo kujua nani anastahili kulipwa kiasi gani na atakapokuja hapa, yule anayeoona hakutendewa haki aje na nyaraka zake zote'' alisema Lukuvi.

Kwa mujibu wa Lukuvi, serikali tayari imeanza kulipa fidia na kubainisha kuwa wale wananchi ambao fidia haikwenda vizuri serikali ipo na kila mtu lazima alipwe kulingana na mali zake na kusisitiza kuwa Rais Samia Suluhu ashatoa fedha kwa ajili ya kujenga huduma za shule, zahanati pamoja na maji.

Aidha waziri Lukuvi alisisitiza kuwa wale waliotakiwa kuhama wahame wakati shauri hilo likiendelea na waende katika maeneo yao waliyopangiwa ili kupisha shughuli zilizopangwa kwa huduma zote za msingi kama shule na zahanati zitawafuata huko waliko.



Umati wa wakati wa Mombose uliojitokeza kuwasikiliza mawaziri wanane wa kamati ya kisekta ukifuatilia kwa makini maelezo yaliyokuwa yanatolewa na mwenyekiti wa kamati hiyo Mhe. Lukuvi.



Bibi Jeniffer Emanuel, akiwasilisha malalamiko yake ya kulipwa fidia ndogo ya nyumba yake isiyoendana na gharama halisi na kumwomba Waziri Lukuvi kusaidia ili aweze kupata haki.



Bwana James Mahina akiielezea kamati kuwa amelipwa kiasi cha shilingi 50,000 tu kwa heka moja ambayo sio gharama halisi ya eneo hilo ambapo hivi sasa heka moja inauzwa shilingi 750,000.

# MKUNGUNERO KUFANYIWA TATHMINI UPYA

**Na Munir Shemweta, WANMM Kondoa**



*Waziri wa Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi William Lukuvi akizungumza na wakazi wa kijiji cha Bereko wilayani Kondoa mkoa Dodoma wakati wa ziara ya mawaziri wa kisekta kutafuta ufumbuzi wa migogoro ya ardhi kwenye maeneo ya hifadhi tarehe 6 Oktoba 2021.*

Waziri wa Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi William Lukuvi amesema timu ya wataalamu itapelekwa katika Pori la Akiba la Mkungunero lililopo wilayani Kondoa mkoa wa Dodoma kufanya tathmini na kuweka mipaka upya kwa lengo la kuepusha kuvamiwa.

Waziri Lukuvi alibainisha hayo tarehe 6 oktoba 2021 wilayani Kondoa mkoani Dodoma wakati akizungumza na wakazi wa kijiji cha Bereko akiwa katika ziara ya Mawaziri wa kisekta ya kutoa mrejesho wa utatuzi wa migogoro ya matumizi ya ardhi katika vijiji 920.

“Katika Pori la Akiba la Mkungunero tutafanya tathmini upya na kuweka mipaka upya ili wananchi wajue eneo lililohifadhiwa linaanzia wapi na linaishia wapi” alisema Lukuvi.

Kwa mujibu wa Waziri Lukuvi, baada ya kufanyika tathmini upya na mipaka kupimwa hatarajii kuona wananchi wakivamia maeneo ya hifadhi na mapori ya akiba na kueleza kuwa, Rais Samia Suluhu Hassan ameamua kumaliza migogoro ya matumizi ya ardhi katika maeneo mbalimbali nchini.

Akielezea mgogoro wa matumizi ya ardhi eneo la Bereko wilayani Kondoa, Lukuvi alisema, eneo hilo halina mgogoro mkubwa ukilinganisha na maeneo mengine kwa kuwa mgogoro uliopo unaohusisha ekari 17.2 pekee.

Hata hivyo, Waziri wa Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi aliwataka wakazi wa Bereko kujiepusha na tabia ya kuvamia maeneo ya vyanzo vya maji na kubainisha kuwa, serikali haitasita kuwaondoa watakaojenga kandokando ya mito.

Mapema Mbunge wa jimbo la Kondoa ambaye ni Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia Dkt. Ashatu Kijaji aliueleza ujumbe wa Mawaziri nane wa kisekta kuwa wananchi wa eneo la Bereko wana tatizo na msitu wa TFS kwenye mlima Salanka aliouleza kuwa mipaka yake imekuwa haitabiriki kutokana na kuhamahama.

“Msitu katika Mlima Salanka umekuwa kero na wananchi wanaumizwa, msitu una mipaka isiyotabirika kwa kuwa inahamahama na wakati mwingine inasogezwa kwenye mbaazi” alisema Dkt Ashatu.

Timu ya Mwaziri nane ikiongozwa na Waziri Lukuvi imemaliza ziara yake kwenye mkoa wa Dodoma katika wilaya ya Kondoa kwa kutembelea vijiji na mitaa kwenye pori la akiba la Swagaswaga na vijiji vilivyopo kinga la mita 500 katika pori la akiba la Mkungunero na baadaye kuelekea mkoa wa Manyara kuendelea na ziara ya kutoa mrejesho wa utatuzi wa migogoro ya matumizi ya ardhi katika maeneo ya hifadhi.



*Sehemu ya wananchi wa Bereko wilayani Kondoa mkoa wa Dodoma wakifuatilia maelezo yaliyokuwa yakitolewa na Mawaziri wa kisekta wakati wa ziara ya kutafuta ufumbuzi wa migogoro ya ardhi kwenye maeneo ya hifadhi tarehe 6 Oktoba 2021.*



*Mbunge wa Jimbo la Kandoa ambaye ni Waziri wa Habari, Mwasiliano na Teknolojia Dkt Ashatu Kijaji akizungumza wakati wa ziara ya mawaziri wa kisekta kutafuta ufumbuzi wa migogoro ya ardhi katika maeneo ya hifadhi kwenye kijiji cha Bereko wilaya ya Kondoa mkoani Dodoma tarehe 6 Oktoba 2021.*



*Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii Mery Masanja akizungumza na wananchi wa Bereko wilayani Kondoa mkoa Dodoma wakati wa ziara ya mawaziri wa kisekta kutafuta ufumbuzi wa migogoro ya ardhi katika maeneo ya hifadhi tarehe 6 Oktoba 2021.*



*Picha inayoonesha eneo la Pori la Akiba la Mkungunero kwenye kijiji cha Bereko wilaya ya Kondoa mkoani Dodoma*

# WATENDAJI TIMIZENI WAJIBU – MASANJA

## Na Happiness Shayo WMU

Watendaji wa Mikoa, Wilaya, Miji na Vijiji nchini wametakiwa kutekeleza majukumu yao ipasavyo kwa kuhakikisha wanasimamia vizuri maeneo ya hifadhi ili kuepusha migogoro kati ya wananchi na Serikali.

Hayo yamesemwa na Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii Mhe. Mary Masanja (Mb) alipokuwa akizungumza na watendaji wa mkoa wa Singida katika kikao cha Mawaziri 8 chenye lengo la kutatua migogoro ya ardhi kilichofanyika katika Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Singida leo.

"Migogoro ya wananchi kuvamia maeneo ya hifadhi inajitokeza wakati watendaji wenye dhamana na walioajiriwa na Serikali wapo wanatazama tu mpaka inafikia katika hali hii" Mhe. Masanja amefafanua.

Mhe. Masanja ameongeza kuwa mtendaji yeyote atakayehusika katika kusababisha migogoro ya wananchi kwa kutosimamia vizuri eneo lake la kazi hastahili kwenda na kasi ya awamu ya sita na ana mpango wa kurudisha nyuma jitihada za Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan za kutatua migogoro.



*Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mhe. Mary Masanja (Mb) akizungumza na watendaji wa Mkoa wa Singida wakati wa ziara ya kikazi ya Kamati ya Mawaziri 8 wa Kisekta yenye lengo la kutatua migogoro ya ardhi walipotembelea Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Singida leo.*

"Hakikisheni kwamba maeneo yote ya hifadhi ambayo tunayaachia kwa ajili ya wananchi mnayasimamia vizuri ili kumpa nafasi Mhe. Rais kutekeleza majukumu yake vizuri ya kuwahudumia wananchi.

Ameongeza kuwa migogoro hiyo ambayo Mhe. Rais Samia Suluhu Hassan ameisimamia na kutoa suluhu yake kwa kuiagiza Kamati ya Mawaziri 8 wa Kisekta kuitatua si vyema ikajirudia.



*Kamati ya Mawaziri 8 wa Kisekta ikiongozwa na Mwenyekiti ambaye ni Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mhe. William Lukuvi (Mb) (katikati) ikimsikiliza Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mhe. Mary Masanja (Mb) (hayupo pichani) alipokuwa akizungumza na watendaji wa Mkoa wa Singida leo.*



*Baadhi ya watendaji kutoka katika Wizara mbalimbali za Kisekta wakimsikiliza Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mhe. Mary Masanja (Mb) (hayupo pichani) alipokuwa akizungumza na watendaji wa Mkoa wa Singida leo.*



*Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mhe. Mary Masanja (Mb) akitia saini kitabu cha wageni wakati wa ziara ya kikazi ya Kamati ya Mawaziri 8 wa Kisekta yenye lengo la kutatua migogoro ya ardhi walipotembelea Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Singida leo.*



*Naibu Katibu Mkuu, Wizara ya Maliasili na Utalii, Ludovick Nduhiye akifuatilia mada wakati wa ziara ya kikazi ya Kamati ya Mawaziri 8 wa Kisekta yenye lengo la kutatua migogoro ya ardhi walipotembelea Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Singida leo.*

# HATUSAJILI VIJIJI BILA KUSHIRIKISHA WADAU MUHIMU- MHE. SILINDE

**Na. Munir Shemweta WANMM TABORA**

Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) David Silinde amesema kuanzia sasa ofisi yake haitasajili vijiji bila kushirikisha wadau muhimu ili kuondokana na migogoro ya matumizi ya ardhi inayojitokeza Hatua hiyo ni kutaka kuondoa mgongano uliojitokeza wakati wa kushughulikia migogoro ya matumizi ya ardhi kwenye vijiji 975 ambapo ilibainika baadhi ya vijiji kusajiliwa ndani ya mipaka ya hifadhi.

''Mhe Rais Samia Suluhu Hassan ameelekeza TAMISEMI iwe inashirikisha wadau muhimu wakati wa kusajili vijiji ili kuondokana na migogoro ya matumizi ya ardhi iliyojitokeza kwenye vijiji 975'' alisema Silinde.

Kwa mujibu wa Naibu Waziri TAMISEMI, wakati Kamati ya Mawaziri nane ikishughulikia migogoro ya matumizi ya ardhi, baadhi ya vijiji vimeonekana kuwa ndani ya hifadhi na wananchi wake wamekuwa wakishiriki chaguzi mbalimbali zikiwemo zile za za serikali za mitaa.



*Naibu Waziri Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa David Silinde akizungumza katika moja ya mikutano ya Mawaziri wa Kisekta kutoa mrejesho wa utekelezaji wa maamuzi ya Baraza la Mawaziri kuhusiana na utatuzi wa migogoro ya matumizi ya ardhi katika vijiji.*

Wadau muhimu watakaoshirikishwa katika usajili wa vijiji ni pamoja na Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira, Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Wizara ya Ulinzi pamoja na Wizara ya Maliasili na Utalii.

''Ofisi ya rais TAMISEMI ndiyo inayohusika na usajili wa vijiji lakini kutokana na matatizo yaliyojitokeza kwenye migogoro hii ya vijiji 975 kuanzia sasa hatutasajili tena kijiji mpaka tuwasiliane na sekta nyingine kama vile Wizara ya Maliasili na Utalii, Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi pamoja na Wizara ya Ulinzi'' alisema Silinde.

Akizungumza mkoani Tabora tarehe 12 Oktoba 2021 Silinde alisema, kutoshirikisha wadau muhimu wakati wa kusajili vijiji kumesababisha kuwepo vijiji ndani ya maeneo ya hifadhi na hivyo kuchangia migogoro ya matumizi ya ardhi.

Wakati wa kushughulikia migogoro ya matumizi ya ardhi katika vijiji 975 Kamati ya Mwaziri inayoongozwa na Waziri wa Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi William Lukuvi ilibaini baadhi ya vijiji kusajiliwa ndani ya mipaka ya hifadhi na kuwa na miundombinu ya kijamii.

Akielezea utekelezaji wa maamuzi ya Baraza la Mawaziri kuhusu utatuzi wa migogoro ya matumizi ya ardhi kwenye vijiji 975, Waziri wa Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi William Lukuvi alisema, mkoa wa Tabora unahusisha vijiji 100 na ni mkoa wenye vijiji vingi ukilinganisha na mikoa mingine ambapo vijiji 94 kati ya hivyo ndivyo vitakavyobaki na maeneo yake kama yalivyo.

Kwa mujibu wa Lukuvi, mchanganuo wa utekelezaji maamuzi Baraza la Mawaziri ni kuwa vijiji 50 vilivyosajiliwa ndani ya hifadhi vitaendelea na hadhi yake huku vijiji 15 migogoro yake ikiwa tayari imetatuliwa na kijiji kimoja vitongoji vyake vitabaki kwenye hifadhi .

Aidha, alisema kuna vijiji 11 vitakavyomegewa maeneo katika hifadhi na vijiji 17 vilivyokuwa na migogoro ya mipaka na hifadhi vitabaki lakini mipaka yake itarejewa kwa njia shirikishi.

''Rais wa Jamhuri ya ,Muungano wa Tanzania Samia Suluhu Hassan ametuelekeza tutekeleze uamuzi huu kwa umakini mkubwa bila ya kuleta taharuki kwa wananchi na kwa kuzingatia maslahi mapana ya wananchi na Taifa kwa ujumla'' alisema Lukuvi.



*Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi mkoa wa Tabora Hassan Wakasuvi akizungumza katika mkutano wa Mawaziri wa Kisekta kutoa mrejesho maamuzi ya Baraza la Mawaziri kuhusiana na utatuzi wa migogoro ya matumizi ya ardhi katika vijiji mkoa wa Tabora.*



*Wananchi wa kijiji cha Kigwa wilayani Uyui mkoani Tabora wakifurahia uamuzi wa kijiji hicho kumegewa sehemu ya ardhi ya Hifadhi ya Kigwa-Rubuga wakati wa ziara ya Kamati ya Mawaziri wa Kisekta kuhusiana na utatuzi wa migogoro ya matumizi ya ardhi katika vijiji 975.*



*Sehemu ya Mawaziri wa Wizara za Kisekta wakiwa katika mkutano wa wananchi katika kijiji cha Kigwa wilayani Uyui mkoa wa Tabora. Wa nnne kushoto ni Mkuu wa mkoa wa Tabora Dkt Batilda Burian.*

# TABORA WANUFAIKA NA ZIARA YA KISEKTA



Wazairi wa Mifugo na Uvuvi Mhe. Mashimba Ndaki akiongea na wananchi wa vijiji vya Tabora juu ya maeneo yao yatayotengwa kwa ajili ya ufugaji.









## Na Munir Shemweta, WANMM Tabora



Wazairi wa Mifugo na Uvuvi Mhe. Mashimba Ndaki amesema mkoa wa Tabora ni wanufaika wakubwa katika utekelezaji wa maamuzi ya Baraza la Mawaziri kuhusiana na utatuzi wa migogoro ya matumizi ya ardhi katika vijiji 975 nchini.

Katika utekelezaji maamuzi ya Baraza la Mawaziri kuhusiana na utatuzi wa migogoro ya matumzi ya ardhi katika vijiji, Mkoa wa Tabora unahusisha vijiji 100 ikiwa ni mkoa wenye vijiji vingi ukilinganisha na mikoa mingine ambapo vijiji 94 kati ya hivyo ndivyo vitakavyobaki na maeneo yake kama yalivyo.

''Mkoa wa Tabora ni wanufaika wakubwa na utatuzi huu wa migogoro ya matumizi ya ardhi kwa kuwa una wafugaji na ngombe nyingi'' alisema Mhe. Ndaki.

Kwa mujibu wa Waziri wa Mifugo na Uvuvi Mhe. Mashimba Ndaki iwapo tatizo la migogoro ya ardhi katika mkoa wa Tabora litapatiwa ufumbuzi basi wafugaji wataweza kuhifadhi mifugo yao na kwa sehemu kubwa litakuwa limepata tiba.

Katika mkoa wa Tabora misitu ya hifadhi minne imefutwa kwa ajili ya kuipanga na kugawiwa kwa wananchi kwa shughuli za ufugaji, kilimo na makazi huku baadhi ya vijiji vilivyoingia ndani ya hifadhi vikimegewa sehemu ya hifadhi kwa ajili ya kupatiwa wananchi ili kuendesha shughuli za kiuchumi.

# SITAKUWA KIKWAZO KWENYE UPATIKANAJI WA MAJI – AWESO

## Na Lusajo Mwakabuku NZEGA

Waziri wa Maji Mhe. Juma Aweso amesema hatakuwa kikwazo katika kuhakikisha maji safi na salama yanapatikana katika maeneo yote ambayo wananchi wanahamishiwa na mipango bora ya matumizi inapangwa ili wananchi waendelee kuhangaikia shughuli nyingine za maendeleo badala ya kusafiri umbali mrefu kufuata maji au kutumia maji yasiyo salama.

Kauli hii ya Mhe. Aweso imekuwa ni kauli mbiu kwa kila kijiji ambacho yeye pamoja na kamati ya mawaziri wenzake ya kisekta 8 wanaendelea na ziara katika mikoa 10 nchini kwa lengo la kutatua migogoro inayohusiana na matumizi ya ardhi ambapo kamati hii inatekeleza majukumu yake katika vijiji 975 nchini.

Akiongea na wananchi wa kijiji cha kilichopo katika jimbo la Nzega vijijini Waziri Aweso amesema Mhe. Rais Samia Suluhu Hassan ametenga fedha nyingi kwa ajili ya maji na nzega tayari ina miradi ya kutosha ya maji na tayari mkandarasi ameshapatikana kwa ajili ya kuanza kazi ya kuchimba visima.

Aidha Aweso aliongeza kuwa ili kuwahakikishia kuwa maneno yake sio propaganda hivi karibuni atatia sahihi ya makubaliano ya kuanza kwa mradi mkubwa wa maji na kwamba tukio hili litafanyika mkoani Tabora na kushuhudiwa na wana Tabora wenyewe.

Katika hatua nyingine waziri Aweso akiwa Dodoma katika kijiji cha Mombose alisema Rais Samia Suluhu Hassan ametoa kiasi cha shilingi Bilioni 7.7 kwa ajili ya miradi ya maji katika wilaya ya Chemba na kwaomba wananchi kutoa ushirikiano wa kutosha mara kazi hiyo itapoanza ikiwa ni pamoja na kupisha maeneo ambayo tayari wamshalipwa fidia ili kazi ziweze kuendelea.

Mhe. Juma Aweso ni mmoja kati ya mawaziri wanane wanaounda kamati ya kisekta inayoambatana na makatibu wakuu wa wizara za kisekta na wataalamu wa wizara hizo, ikitembelea mikoa 10 kwa awamu ya kwanza na baadaye mengine 16 iliyosalia.



*Waziri wa Maji Mhe. Juma Aweso akiongea na wananchi wa kijiji cha Msondoko wilayani Kondoa juu ya mipango ya maji.*



*Waziri wa Habari na Teknolojia ya mawasiliano na mbunge wa jimbo la Kondoa Mhe. Ashatu Kijaji akitoa shukrani huku akiwa amekaa na wananchi wake akimsikiliza Waziri wa Maji (Hayupo Pichani) akitoa taarifa za miradi ya maji.*



*Mhe. Juma Aweso mmoja kati ya mawaziri wanane wanaounda kamati ya kisekta ya kutatua migogoro ya matumizi ya ardhi akiwaahidi wananchi wa Tabora kuwa mradi mkubwa wa maji utaanza hivi karibuni.*



*Mhe. Juma Aweso akinong'onezana jambo na mwenyekiti wa kamati hiyo Mhe. Lukuvi kabla ya kusimama na kuwasalimia wananchi wa Mkoa wa Manyara wakati ziara ya mawaziri hao ilipokuwa inaendelea.*

# MGOGORO NA MAZINGIRA NI JANGA KUBWA.

*(Ukuni wa masika hatumwi mtoto – Chande)*

**Na. Lusajo Mwakabuku WANMM KITETO**

Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) David Silinde amesema kuanzia sasa ofisi yake haitasajili vijiji bila kushirikisha wadau muhimu ili kuondokana na migogoro ya matumizi ya ardhi inayojitokeza

Hatua hiyo ni kutaka kuondoa mgongano uliojitokeza wakati wa kushughulikia migogoro ya matumizi ya ardhi kwenye vijiji 975 ambapo ilibainika baadhi ya vijiji kusajiliwa ndani ya mipaka ya hifadhi.

"Mhe Rais Samia Suluhu Hassan ameelekeza TAMISEMI iwe inashirikisha wadau muhimu wakati wa kusajili vijiji ili kuondokana na migogoro ya matumizi ya ardhi iliyojitokeza kwenye vijiji 975" alisema Silinde.

Kwa mujibu wa Naibu Waziri TAMISEMI, wakati Kamati ya Mawaziri nane ikishughulikia migogoro ya matumizi ya ardhi, baadhi ya vijiji vimeonekana kuwa ndani ya hifadhi na wananchi wake wamekuwa wakishiriki chaguzi mbalimbali zikiwemo zile za za serikali za mitaa.

Wadau muhimu watakaoshirikishwa katika usajili wa vijiji ni pamoja na Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira, Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Wizara ya Ulinzi pamoja na Wizara ya Maliasili na Utalii.

"Ofisi ya rais TAMISEMI ndiyo inayohusika na usajili wa vijiji lakini kutokana na matatizo yaliyojitokeza kwenye migogoro hii ya vijiji 975 kuanzia sasa hatutasajili tena kijiji mpaka tuwasiliane na sekta nyingine kama vile Wizara ya Maliasili na Utalii, Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi pamoja na Wizara ya Ulinzi" alisema Silinde.

Akizungumza mkoani Tabora tarehe 12 Oktoba 2021 Silinde alisema, kutoshirikisha wadau muhimu wakati wa kusajili vijiji kumesababisha kuwepo vijiji ndani ya maeneo ya hifadhi na hivyo kuchangia migogoro ya matumizi ya ardhi.

Wakati wa kushughulikia migogoro ya matumizi ya ardhi katika vijiji 975 Kamati ya Mwaziri inayoongozwa na Waziri wa Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi William Lukuvi ilibaini baadhi ya vijiji kusajiliwa ndani ya mipaka ya hifadhi na kuwa na miundombinu ya kijamii.

Akielezea utekelezaji wa maamuzi ya Baraza la Mawaziri kuhusu utatuzi wa migogoro ya matumizi ya ardhi kwenye vijiji 975, Waziri wa Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi William Lukuvi alisema, mkoa wa Tabora unahusisha vijiji 100 na ni mkoa wenye vijiji vingi ukilinganisha na mikoa mingine ambapo vijiji 94 kati ya hivyo ndivyo vitakavyobaki na maeneo yake kama yalivyo.

Kwa mujibu wa Lukuvi, mchanganuo wa utekelezaji maamuzi Baraza la Mawaziri ni kuwa vijiji 50 vilivyosajiliwa ndani ya hifadhi vitaendelea na hadhi yake huku vijiji 15 migogoro yake ikiwa tayari imetatuliwa na kijiji kimoja vitongoji vyake vitabaki kwenye hifadhi .

Aidha, alisema kuna vijiji 11 vitakavyomegewa maeneo katika hifadhi na vijiji 17 vilivyokuwa na migogoro ya mipaka na hifadhi vitabaki lakini mipaka yake itarejewa kwa njia shirikishi.

"Rais wa Jamhuri ya ,Muungano wa Tanzania Samia Suluhu Hassan ametuelekeza tutekeleze uamuzi huu kwa umakini mkubwa bila ya kuleta taharuki kwa wananchi na kwa kuzingatia maslahi mapana ya wananchi na Taifa kwa ujumla" alisema Lukuvi.



*Naibu Waziri Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira Mhe. Hamad Chande akiongea na wananchi wa kata ya Makame wilayani Kiteto katika mkoa wa Manyara.*

# MATUKIO KATIKA PICHA











